

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Barua pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Faksi +255262963117



Mji wa Serikali
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S.L.P 2996,
40478 DODOMA,

TAARIFA KWA UMMA

**MKUTANO WA MAJADILIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA
BINAFSI**

01 FEBRUARI, 2023 – DODOMA

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na Wadau katika Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara imeandaa Mkutano wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi utakaofanyika tarehe 02 Februari, 2023.

Mkutano huu unatarajia kufanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (Julius Nyerere International Conference Centre – JNICC) uliopo Jijini Dar es Salaam.

Mkutano unalenga kufanya majadiliano ya namna ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa lengo la kukuza uchumi na kuchochlea maendeleo ya Taifa. Hatua hiyo, inaakisi dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kukuza na kuimarisha majadiliano na ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mkutano wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2023 una Kauli mbiu isemayo: ***“Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji kwa Maendeleo ya Uchumi wa Tanzania”***. Kauli mbiu hii inalenga kuongeza kasi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuifanya sekta binafsi kuwa injini ya uchumi wa nchi.

Mkutano huo utakua na washiriki zaidi ya 500 ukijumuisha Viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Viongozi Wakuu kutoka Serikali ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waheshimiwa Mawaziri wa Kisekta, Makatibu Wakuu wa Wizara za kisekta, Wenyeviti wa Kongani mbalimbali, wamiliki wa kampuni, wamiliki wa viwanda, Vyama vya Sekta Binafsi, Jumuiya za Wafanyabiashara, wawekezaji, wafanyabiashara wadogo

na wa kati, Wakuu wa Taasisi za Serikali, watafiti wabobezi, watunga sera, washirika wa maendeleo na Asasi za Kiraia (AZAKI).

Ili kuendelea kukuza biashara na uwekezaji nchini, Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara nchini (MKUMBI) na kuboresha upatikanaji wa miundombinu na huduma wezeshi kama vile gesi asilia, ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, umeme, maji na ardhi kwa uwekezaji.

Mgeni Rasmi na Mzungumzaji Mkuu anatarajiwu kuwa Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

MWISHO

Imetolewa na:

.....

**KATIBU MKUU
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**